

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI
SHULE YA SEKONDARI MBWEGO**

Kumb. Na MBG/JI/01/16

JINA LA MWANAFUNZI _____

SHULE YA MSINGI _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kuanzia Januari 2021. Ni matumaini yangu kuwa nawe umefurahi kupata nafasi hiyo. Siku ya kuripoti shuleni ni tarehe 11 Januari 2021. Hakikisha unakuja na mzazi/mlezi wako na kama utapanga chumba mtaani uje pia na mwenye nyumba ulipopanga. Ukishindwa kuripoti ndani ya wiki moja kuanzia tarehe 11/1/2021 hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwako na kwa mzazi au mlezi.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

A. SARE ZA SHULE

(i) *Wavulana*

Shona suruali 2 za rangi ya damu ya mzee zisiwe modo, nunua shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi. Suruali ziwe na mifuko mitatu na zisishonwe kihuni na lazima zivaliwe na mkanda mweusi wenye bekonni ndogo. Tai za rangi ya damu ya mzee 2, viatu vyeusi jozi mbili vya kamba na soksi nyeusi jozi 2.

(ii) *Wasichana*

Shona sketi mbili za rangi ya damu ya mzee rinda box, nunua shati mbili nyeupe za mikono mifupi, sketi ilizidi urefu wa inchi 2 chini ya magoti, tai mbili za rangi ya damu ya mzee, soksi jozi mbili nyeupe zisizo na mapambo, viatu vyeusi vya kamba jozi mbili visivyo na visigino virefu, viatu vya bajaji au plastiki haviruhusiwi. Vazi la hijabu linaruhusiwa na lifanane na sare ya shule na livaliwe kwa utaratibu unaotakiwa.

ANGALIZO

Nguo zitakazo shonwa tofauti na sare ya shule hazitakubaliwa

B. VIFAA VYA DARASANI.

- (i) Daftari kaunta 10 za quire 3 (Qr3)
- (ii) Daftari ndogo (book twelve) 6
- (iii) Mkebe wa mahesabu
- (iv) Kalamu za kutosha, penseli na rula
- (v) Kamusi ya kiingereza (English to English Dictionary)

- (vi) Begi la kubebea vifaa vya darasani

C. MUHIMU:

- (i) Ni lazima kuwasiliana kwa kutumia lugha ya kiingereza muda wote, ili uweze kuwasiliana kwa kiingereza itabidi ujifunze kwa bidii.
- (ii) Kama mwanafunzi zingatia nidhamu na kujifunza kwa bidii.
- (iii) Mzazi ahudhurie vikao vya wazazi bila kukosa wala kuwakilishwa.

D. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

- (i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (iii) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparations)
- (iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kwa ukamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (vi) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- (vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote kama inavyotakiwa
- (viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

E. MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, ugolo n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuo au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi shuleni

F. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu
 - (a) Medica Examination form ambayo itajazwa na mganga wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
 - (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
 - (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule
 - (d) Lete nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) au kama huna leta hati ya kiapo kutoka mahakamani (AFFIDAVIT).

KARIBU SANA MBWEGO

Charles D. Kiondo
MKUU WA SHULE
0759 129 579